## **MAELEZO YA MLALAMIKAJI** *baada ya Amri ya RFA kutolewa:*

Mahakama imetoa Amri ya Mwisho inayokusudiwa kukukinga dhidi ya unyanyasaji. **Mshtakiwa anaweza kushtakiwa kwa jinai katika mahakama ya jinai ikiwa mshtakiwa atakiuka amri hiyo.**

Ijapokuwa amri ya mwisho imetolewa, bado mawasiliano yanaweza kufanywa na wakili kutoka wakala wa mashauri ya ukatili wa majumbani wa eneo lako. Kwa maelezo kuhusu wakili katika eneo lako tembelea tovuti hii https://vtnetwork.org/get-help/

**KUARIFIWA.** Kawaida, Mshtakiwa hukabidhiwa mkononi nakala ya Amri ya Mwisho kabla hajaondoka kwenye mahakamani. Ikiwa Mshtakiwa hakuwapo au hilo halikutokea, ni jukumu la Mahakama kuvipatia vyombo vya kisheria vimuarifu/vimfikishie Mshtakiwa. Ikiwa mshtakiwa hajafikishiwa yeye binafsi, Amri haitatekelezwa, na usalama wako unaweza kuwa hatarini.

**UTEKELEZAJI.** Amri zote zinamkataza Mshtakiwa kukunyanyasa wewe na/au watoto wako. Kutegemea na amri yako inasemaje, Mshtakiwa anaweza kuruhusiwa kuwasiliana na wewe au kuwa karibu na wewe, nyumba yako, kazini, shuleni au kwenye gari. Unapaswa kutoa taarifa polisi mara moja kunapotokea ukiukaji wowote wa Amri hiyo. WATAKUSAIDIA KUKAZIA AMRI YAKO. Tunza nakala. Unaweza kupata nakala za ziada kutoka mahakamani.

**UWANDA.** Maafisa wote wa vyombo vya kisheria wanaweza kuangalia orodha ya nchi nzima ili kuona kama Amri yako inatumika na ni nini masharti yake. Amri yako inatekelezwa jimboni kote na nchi nzima.

**KUIELEWA AMRI YAKO.** Unahitaji kusoma Amri yako na kuielewa. Amri hiyo ni DHIDI YA MSHTAKIWA TU. Hii inamaanisha kuwa ni Mshtakiwa tu ndiye anayeweza kukiuka Amri na kukamatwa. Haupaswi kuhimiza mawasiliano na Mshtakiwa ikiwa ameamriwa asiwasiliane nawe. Shauri lolote la jinai dhidi ya mshtakiwa ni tofauti na kesi hii ya RFA. Amri hii ya Korti ya Familia haitabadilisha masharti yoyote ya mahakama ya jinai ya kutolewa au masharti ya msamaha dhidi ya Mshtakiwa. Mabadiliko au kufutwa kwa Amri hii ya RFA halibadilishi masharti ya mshtakiwa kuachiliwa au masharti ya msamaha.

**MABADILIKO KWA AMRI.** MAHAKAMA PEKEE NDIYO INAWEZA KUBADILI AU KUTUPILIA MBALI AMRI. Amri haiwezi kubadilishwa nawe, na Mshtakiwa au kwa makubaliano ya pande zote mbili. Inaweza kubadilishwa tu baada ya ombi la maandishi kuwasilishwa mahakamani na uamuzi kutolewa na Jaji. Jaji anaweza kuhitaji kusikiliza kabla ya kufanya mabadiliko yoyote kwa amri iliyopo.

**MAWASILIANO.** Endapo unahitaji kuwasiliana na Mshtakiwa na yeye haruhusiwi kuwasiliana nawe, Jaji lazima abadilishe Amri kabla Mshtakiwa hajawasiliana nawe.

**VITU BINAFSI.** Amri yako linaweza kukuruhusu wewe au Mshtakiwa kuchukua vitu binafsi kutoka nyumbani. Hiyo inapaswa kutokea tu kwa njia ambayo Amri inaruhusu. Wasiliana na polisi wa eneo lako kwa msaada.
Unaweza kulazimika kulipia huduma hii.

**KUMALIZIKA KWA MUDA.** Tafadhali kumbuka tarehe ya kumalizika kwa Amri yako kwenye ukurasa wa mwisho. Kama unataka kuongeza muda wa Amri mbele ya tarehe ya kumalizika muda, lazima usajili ombi kwa maandishi Mahakamani. Hakikisha unasajili/kuomba wiki chache kabla ya Amri kumalizika.

**WATOTO.** Ili mahakama ishughulikie vizuri na kikamilifu mahitaji ya watoto ya muda mrefu, utahitaji kufungua shauri la Uzazi, Talaka, Utengano, au kesi ya Kuvunja Ndoa. Masharti yoyote ya utunzaji au ya kutembelea katika Amri hii ya RFA yatakoma pale Amri itakapoisha muda wake.

**MALI.** Ili kupata amri ya mwisho juu ya haki za umiliki au umiliki, utahitaji kufungua shauri la Talaka, Kutengana, au kuvunja ndoa kama umeolewa/umeoa au uko katika ndoa ya kisheria. Ikiwa hujaolewa/hujaoa au uko katika ndoa ya kisheria, kupata amri ya mwisho juu ya umiliki wa mali, utahitaji kufungua madai madogo au kesi ya madai katika Mahakama Kuu.

**FOMU.** Waulize wafanyakazi wa mahakama kuhusu fomu, au nenda kwenye www.vermontjudiciary.org .

**MAELEZO YA MSHTAKIWA** *baada ya Amri ya RFA kutolewa:*

Korti imetoa Msaada wa Mwisho wa Amri dhidi ya Unyanyasaji. **UNAWEZA KUSHITAKIWA KWA UHALIFU KATIKA MAHAKAMA YA UHALIFU UKIKIUKA AMRI HII.**

**KUIELEWA AMRI YAKO.** Unahitaji kuisoma Amri na uelewe hasa inachosema ili usiivunje. Ikiwa huielewi, unaweza kutafuta msaada wa kisheria. Tunza nakala. Unaweza kupata nakala za ziada kutoka mahakamani.

**UTEKELEZAJI.** Amri hiyo ni DHIDI YAKO TU. Ni wewe tu unayeweza kukiuka. Ukifanya hivyo, unaweza kukamatwa. UTEKELEZAJI AMRI HIYO UTAKAZIWA NA POLISI.

**NINI CHA KUFANYA.** Ikiwa umeamriwa kukaa umbali maalum kutoka kwa Mlalamikaji na ukatangamana naye kwenye kadamnasi kwa bahati mbaya, lazima uvuke barabara, uondoke dukani au uondoke kwenye hali hiyo mara moja. Ikiwa Amri hairuhusu mawasiliano ya simu na Mlalamikaji anakupigia simu, kata simu.

**MABADILIKO KWA AMRI.** MAHAKAMA PEKEE NDIYO INAWEZA KUBADILI AU KUTUPILIA MBALI AMRI. Amri haiwezi kubadilishwa na Mlalamikaji, nawe, au kwa makubaliano ya pande zote mbili. Inaweza kubadilishwa tu baada ya ombi la maandishi kuwasilishwa mahakamani na uamuzi kutolewa na Jaji. Jaji anaweza kuhitaji kusikiliza kabla ya kufanya mabadiliko yoyote kwa amri iliyopo.

**UWANDA.** Maafisa wote wa vyombo vya kisheria wanaweza kuangalia orodha ya nchi nzima ili kuona kama Amri hiyo inatumika na ni nini masharti yake. Amri yako inatekelezwa jimboni kote na nchi nzima.

**AMRI ZA JINAI.** Shauri lolote la jinai dhidi yako ni tofauti na kesi hii ya RFA. Amri hii ya Korti ya Familia haitabadilisha masharti yoyote ya mahakama ya jinai ya kuachiliwa au masharti ya msamaha kwenye Mahakama ya Wilaya (jinai). Marekebisho ya Amri hii ya RFA, au kufutwa kwake, hayatabadilisha masharti yako ya kuachiliwa au masharti ya msamaha.

**SILAHA ZA MOTO.** Ikiwa utanunua au una bunduki au risasi, unaweza kushtakiwa kwa kosa la jinai la shirikisho. Ikiwa una maswali yoyote kuhusu hili, unaweza kutaka kupata msaada wa kisheria.

**UHAMIAJI.** Kama wewe si raia wa Marekani, Amri hiyo inaweza kuathiri haki yako ya kubaki katika nchi hii. Ikiwa wewe ni raia, inaweza kuathiri haki yako ya kusafiri nje ya nchi. Unaweza kutaka kupata msaada wa kisheria.

**VITU BINAFSI.** Amri yako inaweza kukuruhusu kuchukua vitu binafsi kutoka nyumbani. Hiyo inapaswa kutokea tu kwa njia ambayo Amri inaruhusu. Wasiliana na polisi wa eneo lako kwa msaada. Unaweza kulazimika kulipia huduma hii.

**KUMALIZIKA KWA MUDA.** Amri hii itaendelea kutumika hadi tarehe ya kumalizika muda kwenye ukurasa wa mwisho, na itakaziwa utekelezaji wake kama ilivyoandikwa hadi wakati huo.

**WATOTO.** Ili mahakama ishughulikie vizuri na kikamilifu mahitaji ya watoto ya muda mrefu, utahitaji kufungua shauri la Uzazi, Talaka, Utengano, au kesi ya Kuvunja Ndoa. Masharti yoyote ya utunzaji au ya kutembelea katika Amri hii ya RFA yatakoma pale Amri itakapoisha muda wake.

**MALI.** Ili kupata amri ya mwisho juu ya haki za umiliki au umiliki, utahitaji kufungua shauri la Talaka, Kutengana, au kuvunja ndoa kama umeolewa/umeoa au uko katika ndoa ya kisheria. Ikiwa hujaolewa/hujaoa au uko katika ndoa ya kisheria, kupata amri ya mwisho juu ya umiliki wa mali, utahitaji kufungua madai madogo au kesi ya madai katika Mahakama Kuu.

**FOMU.** Waulize wafanyakazi wa mahakama kuhusu fomu, au nenda kwenye www.vermontjudiciary.org .